


Matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-2012


Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania (THMIS) wa mwaka 2011-12, ulitathmini mikakati ya kuzuia malaria, tiba ya malaria, kiwango cha malaria na upungufu wa damu mwilini.



Nchini Tanzania, 9% ya watoto chini ya miaka mitano walikutwa na malaria walipofanyiwa kipimo cha papo kwa hapo (Rapid Diagnostic Test - RDT). Maambukizi ya malaria yanaongezeka kadri umri unavyoongezeka.

Malaria kwa Watoto (kwa Mikoa)


Asilimia ya watoto wenyewe miezi 6-59 walioonekana kuwa na malaria baada ya kufanyiwa kipimo cha papo kwa hapo (RDT).



Kiwango cha malaria kinatofautiana sana baina ya mikoa. Kiwango cha malaria kiko juu zaidi katika mikoa ya Geita, Kigoma na Lindi.

Kiwango cha Upungufu wa Wastani hadi Mkubwa wa Damu kwa Watoto

Asilimia ya watoto wa umri wa miezi 6-59 wenyewe upungufu wa damu mwilini wa kiwango cha wastani hadi wa kiwango cha juuu (haemoglobin <8.0 g/dl)



Upungufu wa damu ni dalili kubwa ya malaria. Nchini Tanzania, 6% ya watoto chini ya miaka mitano wana upungufu wa damu kiasi hadi upungufu mkubwa wa damu, ambao ni chini ya haemoglobin 8.0/dl. Kwa ujumla, kiwango cha upungufu wa damu wa wastani hadi mkubwa kinapungua sambamba na kuongezeka kwa umri.

Zaidi ya 90% ya wanawake na wanaume wa miaka 15-49 wanafahamu kwamba kuna njia za kujikinga dhidi ya malaria. Njia iliyoitajwa na watu wengi ya kuepuka malaria ni kulala kwenye chandaru.

Umiliki wa Chandarua Kilichotiwa Dawa na Upulizaji Dawa


Asilimia ya:



Katika kaya zote nchini Tanzania, 91% zinamiliki angalau chandarua kimoja kilichotiwa dawa. Umiliki wa chandarua chenyedawa ni mdogo zaidi Mkoa wa Mjini Magharibi (67%) na ni mkubwa zaidi katika Mkoa wa Lindi (96%). Kwa nchi nzima, 14% tu ya kaya ndizo zilizokuwa zimepulizia dawa ndani ya nyumba miezi 12 kabla ya utafiti, lakini 87% ya kaya Zanzibar zilikuwa zimepuliziwa dawa miezi 12 kabla ya utafiti.

Umiliki, Upatikanaji na Utumiaji wa Chandarua chenyedawa

Asilimia ya:




*Kwa makadirio ya chandarua kimoja kwa watu 2

Kaya 9 kati ya 10 zina angalau chandarua kimoja kilichowekwa dawa. Robo-tatu ya wakazi katika kaya wangezeza kulala kwenye chandarua chenyedawa ikiwa kila chandarua kimoja chenyedawa katika kaya kingetumiwa na watu wawili. Kwa ujumla, 68% ya watu katika kaya walilala katika chandarua chenyedawa usiku wa kuamkia siku ya utafiti.

Mwenendo wa Utumiaji wa Chandarua Chenye Dawa

Asilimia ya waliolala kwenye chandarua chenyedawa usiku wa kuamkia siku ya utafiti




Watoto na wajawazito ndio waathirika wakubwa wa malaria. Mwaka 2011-12, 72% ya watoto chini ya miaka mitano na 75% ya wajawazito walilala kwenye chandarua chenyedawa usiku wa kuamkia siku ya utafiti. Matumizi ya chandarua kwa wanakaya, watoto chini ya miaka mitano na wajawazito yameongezeka kwa kiasi kikubwa tangu mwaka 2004-05.

Utafiti wa Viashiria vya VVU/ UKIMWI na Malaria Tanzania (THMIS) 2011-12

Mwenendo wa Tiba ya Kinga ya Malaria kwa Wajawazito


Asilimia ya wanawake waliokuwa wajawazito miaka miwili
kabla ya utafiti, kwa uzazi wao wa mwisho, ambao:



Kuzuia malaria, wajawazito wanapaswa kupatiwa dozi mbili au zaidi za SP/Fansidar wanapokwenda kliniki. Karibu theluthimoja (32%) ya wajawazito walipata tiba hii ya kuzuia malaria (IPTp) walipokwenda kliniki, idadi hii imeongezeka kidogo kutoka 26% katika utafiti wa TDHS wa 2010.

Matibabu ya Homa kwa Watoto

Miongoni mwa watoto chini ya miaka mitano walipata homa wiki mbili kabla ya utafiti, asilimia ya wale ambao:



Zaidi ya nusu (54%) ya watoto waliokuwa wamepata homa walipata dawa za malaria. Miongoni mwa watoto waliokuwa wamepata homa amba walitumia dawa za malaria, 61% walitumia ACT (dawa mseto ya malaria) – tiba inayopendekezwa.

Mwitikio na mfumo wa utafiti: Watoto wote wenye miezi 6-59 wanaishi katika kaya zilizochaguliwa walistahili kupima malaria na kiwango cha damu. Upimaji wa malaria ulifanywa kwa kutumia kipimo cha papo kwa hapo pamoja na kipimo cha kawaida cha kutumia darubini. Upimaji wa kiwango cha damu ulifanywa kwa kutumia kifaa kinachoitwa HemoCue. Kati ya watoto 8,119 walostahili kuingia katika zoezi hilo, 95% walitoa damu kwa ajili ya kipimo cha kiwango cha damu, 94% kwa ajili ya kipimo cha malaria cha papo kwa hapo na 92% kwa kipimo cha malaria cha darubini.

Kwa taarifa zaidi kuhusu matokeo ya Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-12, tafadhalil wasiliana na:

Nchini Tanzania:

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)
P.O Box. 76987, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 212 2651; Nukushi: 255 22 212 2427
www.tacaids.go.tz

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

PO. Box 796, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: 255 22 212 2722; Nukushi: 255 22 213 0852
www.nbs.go.tz

Nchini USA:

ICF International
11785 Beltsville Drive
Calverton, MD 20705 USA
Simu: 301-572-0200; Nukushi: 301-572-0999
www.measuredhs.com
www.statcompiler.com

Malaria

Utafiti wa Viashiria vya VVU/UKIMWI na Malaria Tanzania 2011-12 (THMIS) ulifanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali- Zanzibar (OCGS-Zanzibar) kuanzia Desemba 16, 2011 hadi Mei 24, 2012. Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Zanzibar (ZAC) zilitoa idhini ya kufanyika kwa utafiti huu. Utafiti huu ulifadhiliwa na Shirika la Misaada ya Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID), TACAIDS na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW). ICF International ilisaidia kufanyika kwa utafiti huu kupitia mradi wa MEASURE DHS unaofadhiliwa na USAID. Mradi wa MEASURE DHS unatoa msaada wa kiufundi na fedha kwa tafiti za demografia na afya katika nchi mbalimbali duniani.

